

**MAFUNZO**

Polisi mjini Nakuru kupokea mafunzo namna ya kushughulikia visa vya udhalimu wa kijinsia UK 3



**ELIMU**

Waziri apongeza wakuu wa TVETs kwa mageuzi yaliyosisimua sekta ya elimu UK 10

**KILIMO**

Serikali, sekta ya kibinafsi kushirikiana kuimarisha uzalishaji wa mifugo



UKURASA 4

www.mygov.go.ke

FEBRUARI 21, 2023

# MyGov.

TATHMINI YAKO YA WIKI

TOLEO No. 32/2022-2023

# Serikali kuanzisha tovuti maalumu Kutambua Watu Binafsi mwezi ujao

Katibu wa Uhamiaji na Huduma za Raia, Julius Bittok asema nambari hiyo spesheli itatumiwa kama kitambulisho, Nambari ya Kutambulisha mtu Binafsi, NHIF, na nambari ya KRA na pia kutambua watu wakiwa hai na wakifariki

**NA BERNADETTE KHADULI (KNA)**

Serikali inapanga kuanzisha Nambari Spesheli ya Kutambulisha Mtu Binafsi (UPI) mwezi ujao kunasa na kusajili watoto wote punde tu wanapozaliwa na vifo vinavyotokea nchini.

Kulingana na Katibu wa Uhamiaji na Huduma za Uraia, Balozi Julius Bittok, UPI hiyo itakayopakiwa katika tovuti ya e-Citizen, itapatia watoto wote wanaozaliwa nambari spesheli itakayotumiwa shuleni na vyuoni.



**Katibu, Idara ya Uhamiaji na Huduma za Raia, Julius Bitok akihutubia warsha katika Kenya School of Government, Nairobi.**
**Picha na Bonface Malinda (KNA)**

Katibu Bittok alisema kwamba nambari hiyo spesheli pia itatumiwa kama kitambulisho, nambari ya kibinafsi ya kumtambulisha, nambari ya Bima ya Afya ya Taifa, nambari ya kumtambulisha ya Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru ya Kenya na pia kutambua watu katika maisha yao na wakifariki.

Alisema kwamba kuanzishwa kwa nambari hiyo spesheli ya kumtambulisha kutakomesha zoezi la kitaifa la kuhesabu watu kwa kuwa tekinolojia hiyo mpya itaweza kutoa data sahihi kuhusu idadi ya watu nchini.

"Serikali ya Kenya Kwanza imepatia uraia umuhimu, kwa kupatia kipaumbele ajenda ya mabadiliko ya dijitali na hii itabadilisha mambo mengi katika nchi yetu," alisema na kuongeza kuwa mageuzi ya tekinolojia nchini, Kenya haiwezi kuachwa nyuma kwa kuwa kinachoendesha uchumi na nchi kwa jumula ni tekinolojia.

Katibu alikuwa akizungumza alipofungua warsha ya kutoa mafunzo kuhusu kuanzishwa Kwa nambari spesheli ya kumtambulisha kwa maafisa wote wa kanda na kaunti wa usajili wa watoto wanaozaliwa na vifo katika Chuo cha Serikali cha Kenya,, Kabete.

ENDELEA UK 2

## Tafuteni vyanzo vipya vya mapato, waziri ahimiza wakuu vyuoni

**NA JANE NGUGI (KNA)**



**Ezekiel Machogu**

Waziri wa Elimu Ezekiel Machogu ameshauri vyuo vikuu vya umma kukoma kutegemea karo vinavyokusanya kama karo na ufadhili wa serikali pekee kwa kuwa hauwezi kuvisaidia kuendelea kutekeleza shughuli zake.

Hivyo basi, Machofu alihimiza taasisi hizo vya masomo ya juu kutafuta mbinu zingine za ufadhili kwa kuwa njia za kawaida za mapato zinaendelea kukauka siku baada ya siku.

Bw Machogu vile vile alisema kwamba wakuu wa taasisi hizo wanapaswa kuwazia kukabiliana na changamoto za sasa za kifedha kupitia mikakati kama vile kuimarisha matumizi ya tekinolojia kupunguza gharama, kusaka masoko mapya, kuimarisha utendaji katika shughuli zake, kutafuta ushirikiano na kupatia kipaumbele mipango ya masomo inavyovutia.

Waziri alisema kwamba ingawa vyuo vikuu vya Kenya vinakumbwa na mzozo wa kifedha, hali hiyo inatoa nafasi kwa taasisi hizo kufikiria

ENDELEA UK 2

**Takwimu za Wiki**

| 109,889 | 35 | 8.89b | 254,000 |
|---|---|---|---|
| Tani za nasi zilizokuzwa Kenya 2019 kulingana na Kenya Bureau of Statistics | Vyuo vikuu vya umma ambavyo vina shida kulipa mishahara kwa kukosa fedha | Gharama ya kiwanda cha Umeme kitakachojengwa na shirika la Japan Nakuru | Idadi ya samaki wadogo serikali ya kaunti ya Kirinyaga imesambazia wakulima |

## Kusambaza upendo wa siku ya Valentino



**Mfungwa wa kike na mwanawe wapokea maua kutoka kwa mhisani katika Eldoret Women siku ya Valentino. Katibu wa Huduma za Kurekebisha Tabia Mary Muthoni asema kesi za kina mama wenye makosa madogo zapasa kuharakishwa kusikizwa.** HABARI KAMILI UK 3

KOMESHA COVID-19
" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"
HOMA KIKOHOZI KUSHINDWA KUPUMUA MAUMIVU KOONI KUUMWA NA KICHWA

# Serikali kuanzisha tovuti Kutambua Watu Binafsi Machi

ENDELEA KUTOKA UK 1

Balozi Bittok alisema kwamba kwa wakati huu, ni asilimia 86 ya idadi ya watoto wanaozaliwa wanasajiliwa huku vifo vikiwa asilimia 60 akisema kwamba baada ya kukumbatia dijitali, idadi inatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 90.

Alielezea imani yake kwamba mfumo wa UPI ambao umekopwa Estonia utaondoa ukaguzi na ubaguzi wa usajili katika kaunti za mpakani, na pia kuruhusu kila Mkenya kupata huduma katika tovuti ya e-Citizen.

"UPI itathibitisha wakati wa kuzaliwa iwapo mtoto ni Mkenya wakati maelezo ya wazazi yanawekwa katika tovuti ya e-Citizen.

Nambari ya UPI inaweza kuonyesha iwapo mtoto ni msichana au mvulana anapozaliwa," alisema Katibu. Aidha, alihimiza maafisa wa usajili kuhakikisha wananasa watoto wote wanaozaliwa na watu wanaofariki katika maeneo yao akisema kwamba serikali imeweka mipango na hospitali kuhusu jinsi ya kurekodi visa hivyo.

> "UPI itathibitisha wakati wa usajili ikiwa mtoto ni raia wa Kenya au la" -Bitok

Alitaja usahihi, utendaji na kuziba mianya katika ukusanyaji wa mapato kunakotokana na mfumo usio wa dijitali kama baadhi ya manufaa ya mfumo wa UUPI Katibu alisema, " Mabadiliko ya Dijitali pia yatanasa pesa na ada zinazolipwa serikali."

Mpango wa serikali ni kupakia huduma 5000 za serikali katika e-Citizen kufikia Juni 30 mwaka huu.



**Katibu, Idara ya Uhamiaji na Huduma za Raia, Julius Bitok ashauriana na Mkurugenzi wa E-Citizen Isaac Ochieng kwenye warsha katika Kenya School of Government, Nairobi.**
**Picha na Bonface Malinda (KNA).**

# Tafuteni vyanzo vingine vya mapato, waziri ashauri vyuo

ENDELEA KUTOKA UK 1

zaidi kwa ubunifu jinsi ya kupata mapato.

Aidha, alishauri taasisi hizo kufikiria upya mikakati ya elimu ya juu na kukumbatia mafunzo ya kiufundi, elimu anuai inayowapa wahitimu uwezo wa kujiajiri na kujipatia mapato.

Machogu pia alisema vyuo vikuu vinafaa kuinua ukusanyaji wa mapato kutoka njia zingine ikiwemo utafiti wenye ushindani, ruzuku za ujasiriamali, vyama vya wanafunzi wa zamani, kuendelea kufunza, huduma kwa jamii na uwekezaji wa biashara.

Bw Machogu alisema kwamba vyuo vikuu vinapaswa kuendelea kuwekeza katika utafiti mkubwa na ubunifu ili kuvutia ufadhili na kuhakikisha ubora wa elimu.

Kwa muda mrefu, vyuo vikuu vimekuwa vikitegemea ufadhili wa serikali na mapato kutoka karo zinazokusanya kutoka kwa wanafunzi wa kujitegemea.

Lakini vilipata pigo kubwa serikali ilipopunguza ufadhili na kufanyia mageuzi mitihani ya kitaifa mwaka wa 2016 kwa kuondoa kozi za kujilipia kwa kuwa wanafunzi wote waliopata alama za kujiunga na vyuo vikuu walisajiliwa chini ya mfumo wa kawaida.

Vyuo vikuu vyote 35 vya umma kwa wakati huu zinakumbwa na matatizo ya kifedha kwa kushindwa kulipa mishahara na pia kulipa pesa zinazokata wafanyakazi. Changamoto hizi zinaonyesha kuwa vyuo vikuu havitekelezi jukumu lake kuu la kufunza, utafiti na mafunzo.

Kwa wakati huu, wafanyakazi wanadai zaidi ya Sh7.9 bilioni, ikiwemo ada za hazina za pensheni.

Waziri alisema hayo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu wa Idara ya Serikali ya Elimu ya Juu na Utafiti Dkt Beatrice Inyangala wakati wa mahafala ya 46 ya Chuo Kikuu cha Egerton.



**Chansea wa Chuo Kikuu cha Egerton Dkt Narendra Raval (kushoto) amtunuku msomi digrii ya PhD kwenye sherehe ya 46 ya kufuzu ya chuo hicho.**

The President's Award - Kenya
Proud to be THE DUKE OF EDINBURGH'S INTERNATIONAL AWARD in Kenya

## TANGAZO LA KAZI

Idara ya Kusimamia Utoaji wa Tuzo za Rais- Kenya (PA-K) ni Shirika lililoanzishwa kwa Sheria ya Bunge, Sheria ya Tuzo ya Rais Nambari 30 ya 2017. Idara ya Kusimamia Utoaji wa Tuzo za Rais-Kenya inalenga kuendeleza na kutoa shughuli bora za uzoefu zinazotoa ujuzi chanya wa maisha na maadili ya kimaadili kwa vijana kwa jamii bora.

Idara imejitolea kuwapa wafanyikazi wake mazingira ya kufanyia kazi ambayo ni ya haki na yanayofaa kwa ukuaji wa taaluma ya mtu binafsi na kufikia malengo na malengo ya shirika.

PA-K inataka kuajiri watu waliohitimu, wenye uzoefu, na wenye uwezo kwa nafasi zifuatazo.

| No. | Kumbukumbu | Jina la Nafasi | Daraja | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | PAK-ACCT/1/2023 | Mhasibu Mkuu | PAK 4 | Nafasi 1 |

**Jinsi ya kutuma ombi:**

I. Watu wanaovutiwa na wanaotimiza mahitaji wanapaswa kujaza fomu ya maombi ya kazi mtandaoni kupitia kiungo hiki: ***https://forms.office.com/r/KzhJ3SBW9w***

II. Zaidi ya hayo, waombaji wanaombwa kuwasilisha Wasifukazi wa hivi karibuni, barua ya kazi, Nakala Ziliz-oidhinishwa za Vyeti vya Masomo na Utaalam, Kitambulisho cha Kitaifa/Pasipoti, Vyeti, na hati zingine muhimu kwa:

**Afisa Mkuu Mtendaji,**
**Idara ya Kusimamia Utoaji wa Tuzo za Rais - Kenya,**
**P.O. Box 62185-00200**
**15 Elgon Road, Upper Hill, Nairobi.**
**recruit@presidentsaward.or.ke**

Maombi yanapaswa kutumwa kupitia posta, barua pepe au kwa mikono, ikionyesha wazi nafasi na nambari ya kumbukumbu ya kazi, kwenye barua ya kazi na bahasha.

Maombi yanapaswa kufikia Idara ya Tuzo za Rais -Kenya mnamo au kabla ya **6 Machi, 2023, saa 5.00 jioni.**

- PA-K ni mwajiri anayetoa nafasi sawa, aliyejitolea kuzingatia utofauti na usawa wa kijinsia. Wanawake na watu wenye ulemavu wanahimizwa kutuma maombi.
- Tutawasiliana na wagombea watakaoorodheshwa pekee.
- Baada ya kupata ajira, mgombea aliyefaulu LAZIMA awasilishe na kukidhi mahitaji ya Sura ya Sita ya Katiba ya Kenya 2010 kwa kutoa nakala za hati zifuatazo;
- Cheti halali cha Kuzingatia Ushuru kutoka kwa Mamlaka ya Kukusanya Ushuru Kenya (KRA);
- Cheti halali cha Maadili Mema kutoka kwa Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI);
- Cheti halali cha Uidhinisho kutokak kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELB);
- Cheti halali cha Uidhinisho kutoka kwa Afisi ya Marejeleo ya Mikopo iliyoidhinishwa (CRB) na
- Fomu halali ya Uidhinisho kutoka kwa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC)
- Ombi la mgombea yeyote atakayepatikana akidanganya litafutiliwa mbali

REPUBLIC OF KENYA
knls Read Know Empower kenya national library service

## NAFASI ZA KAZI

Kenya National Library Service (knls) Board ni shirika la kiserikali ya Kenya lililobuniwa na Sheria ya Bunge, Sura 225 ya Sheria za Kenya mnamo Aprili 1965. Wajibu wa Bodi ni kutengeneza, kukuza na kuweka vifaa vinavyohitajika kwenye maktaba za Kenya. Kifungu cha Sheria, Sura ya 446 kuhusu Mashirika ya Umma pia hutoa maelekezo kuhusu operesheni za Bodi.

Ili kufanikisha majukumu yake, Bodi ya knls ingependa kuajiri Wakenya waliohitimu kujaza nafasi zifuatazo:

| S/ No | Nafasi | Kiwango cha mshahara | Idadi ya video | Masharti ya kazi | Eneo la kazi | Nambari ya marejeleo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Naibu Mkurugeni-Fedha na Usimamizi | 2 | 1 | Permanent & Pensionable | Nairobi | KNL/HQ/AD/180C/VOL.3/69 |
| 2. | Afisa wa Maswala ya Wafanyakazi– ***(Marudio)*** | 4 | 1 | Permanent & Pensionable | Nairobi | KNL/HQ/AD/180C/VOL.3/70 |
| 3. | Afisa Mkuu wa Ununuzi | 4 | 1 | Permanent & Pensionable | Nairobi | KNL/HQ/AD/180C/VOL.3/71 |
| 4. | Mkutubi Mwandamizi | 5 | 1 | Permanent & Pensionable | Garissa | KNL/HQ/AD/180C/VOL.3/72 |
| 5. | Principal Librarian | 5 | 1 | Permanent & Pensionable | Nairobi | KNL/HQ/AD/180C/VOL.3/72 |

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI**

Wale wanaotaka kutuma maombi wanaweza kuingia kwenye wavuti wa knls website **www.knls.ac.ke** kwa maelezo zaidi kuhusu kazi na mahitaji ya kazi mbalimbali kwa nafasi zilizotajwa hapo juu.

Maombi yote yanapasa kutumwa na kupokewa kwenye anwani iliyopo hapa chini kwa njia ya nakala kufikia **Machi 7, 2023 saa 11.00 jioni Majira ya Afrika Mashariki.**

**Mkurugenzi/CEO**
**Kenya National Library Service**
**Maktaba Kuu Building – 5th Floor**
**Ngong Road, Community Area**
**S.L.P 30573-00100NAIROBI**

**Kumbuka:**

***Knls Board ni mwajiri anayezingatia usawa, Walio na Ulemavu, Vijana, Watu kutoka Makundi yaliyobaguliwa na Jamii za Wachache wanaotosheleza mahitaji ya kazi zilizotangazwa wanahimizwa kutuma maombi. Ni wale tu watakaoteuliwa na wale watakaofuzu watahitajika kuleta fomu zilizojazwa kutoka KRA, DCI, EACC, HELB na CRB.***

# Polisi kaunti ya Nakuru kufunzwa jinsi ya kushughulikia kesi za GBV

**NA ANNE MWALE (KNA)**

Shirika la Centre for Rights, Education and Awareness (CREAW) kwa ushirikiano na Huduma ya Taifa ya Polisi litatoa mafunzo kwa maafisa wa polisi kaunti ya Nakuru ambayo yataimarisha jinsi wanavyoshughulikia waathiriwa wa dhuluma za Kingono na Jinsia (SGBV).

Mafunzo hayo, kulingana na Afisa wa Mipango wa CREAW, William Mbanyamlenge, pia yataangazia jinsi ya kuimarisha uhusiano wa umma kati ya maafisa wa polisi na umma kurahisisha mzigo wa waathiriwa kutafuta haki.



**Koplo Samwel Ondimu Ngare azungumza wakati wa kikao cha mashauriano kuhusu bima za mapema na dhuluma za kijinsia dhidi ya wanawake. Picha na Dennis Rasto**

"Tumekuwa na visa ambavyo waathiriwa wanatishwa au kunyanyaswa na maafisa wa polisi wanapoenda kuripoti visa vya dhuluma. Waathiriwa wanaume wakati mwingine huwa wanakejeliwa na kuchongolewa katika vituo vya polisi," alisema Bw Mbanyamlenge. Kulingana na Afisa huyo wa Mipango, mafunzo hayo pia yatahakikisha maafisa wa polisi watafunzwa kikamilifu kuhusu kuandika taarifa na jinsi ya kuchukua sampuli kutoka kwa waathiriwa wa GBV na manusura. Hii, aliongeza, itahakikisha kwamba kesi za GBV ziko na nguvu zinapopelekwa kortini kuhakikisha haki kwa waathiriwa.

Bw Mbanyamlenge alisema hayo Ijumaa iliyopita akiwa Nakuru katika mkutano wa mashauriano kuhusu SGBV na ghasia dhidi ya wanawake uliohudhuriwa na wadau wakiwemo wawakilishi wa Tume ya Kitaifa ya Jinsia na Usawa (NGEC), Huduma ya Taifa ya Polisi, Wizara ya Elimu, Serikali ya Kaunti, na Idara ya Serikali ya Jinsia, miongoni mwa wengine.

Alisema kwamba waathiriwa wa ghasia za nyumbani wataadhulumiwa wakiwa nyumbani, mahali ambapo kwa kawaida panapaswa kuwa salama zaidi; na wanaishia kudhulumiwa kimwili na kisaikolojia na kutengana au kutalikiana miongoni mwa maovu mengine. "Wanawake na watoto wanaotaka kuzungumzia masaibu yao hupata wakati mgumu kwa sababu ya aibu au woga. Wanapopiga ripoti, baadhi ya maafisa wa polisi huchukulia makosa hayo kwa mzaha na kuwaongezea shida," alisema na kuongeza kuwa mafunzo hayo, ambayo baadaye yatapatiwa viongozi wa eneo hilo wakiwemo machifu na manaibu wao yananuiwa kuhamasisha maafisa hao.

> "Wanawake wanaotaka kuzungumza huchelea kufanya hivyo sababu ya uoga," Afisa

Katika baadhi ya vituo vya polisi, aliongeza, Dawati za Jinsia hazishughulikiwi na maafisa waliofunzwa kuhusu kuchunguza visa vya SGBV.

"Kuhamishwa kwa maafisa ni kikwazo kwa sababu wakati mwingine tunawapa mafunzo maafisa ambao wanahamishwa na kupata wengine huchukua muda," alisema.

# Harakisheni kesi za walio na watoto rumande-Katibu

**NA KIPTANUI CHERONO (KNA)**

Serikali inataka kesi zinazohusu akina mama walio na watoto rumande ziharakishwe iwapo kesi zao ni ndogo ili kulinda maslahi ya watoto wasio na hatia. Katibu wa Idara ya serikali ya Huduma za Urekebishaji Tabia Bi Mary Muthoni Muriuki alisema inahuzunisha kwamba watoto hao wasio na hatia wanajipata wakifungiwa katika magereza pamoja na mama zao kwa vipindi virefu ilhali hawana makosa. Alielezea hofu yake kwamba watoto hao hujipata wakichanganyika na watu wazima walio na tabia za kila aina kwa sababu mama zao walivunja sheria.

"Iwapo kesi z mama walio na watoto zinaorodheshwa kama dogo, zinapaswa kuharakisha kuwawezesha kuondoka jela ili watoto wao waweze kujua kama watoto wengine wa kawaida," alisema Katibu. Gereza la wanawake la Eldoret liko na watoto 20 wanaoandamana na mama zzao

Alisema kwamba mbali na kuwa watoto wanaofungiwa gerezani na mama zao hawahusishwi katika bajeti, wanapaswa kutunzwa kwa kupatiwa chakula na mavazi.

Alisema, " Kama Idara ya huduma za urekebishaji, tunashughulikia hili kuhakikisha kuwa watoto hao wanapelekwa sehemu tofauti kwa kuwa wanaweza kujifunza tabia zizofaa wakiwa gerezani."

Alisema hayo alipozuru gereza la Eldoret GK na Kimumu Probation Hostel, Eldoret, ambako watoto wanaovunja sheria wanahifadhiwa kurekebishwa tabia kabla ya kuunganishwa na familia zao.

Katibu alisema kwamba idara inataka kuona matumizi ya mbinu mbadala za kutatua mizozo ili kuhakikisha kesi ndogo zinatatuliwa katika kiwango cha familia au zinaweza kutatuliwa kupitia wawakilishi wa Nyumba Kumi.

National Irrigation Authority

## TENDA WAZI YA KITAIFA

National Irrigation Authority inaalika maombi ya kushiriki tenda zifuatazo:

| S. NO | NAMBARI YA TENDA | JINA LA TENDA | TAREHE YA MWISHO | WASHIRIKI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | NIA/T/162/2022-2023 | Tenda ya utoaji huduma za ulinzi, Ving'ora na Usalama kwa kipindi kati ya Aprili 1, 2023 – Machi 31, 2024 | MachI 3, 2023 saa 6.00 mchana | JUMLA |

Stakabadhi yenye maelezo kamili ya tenda ikiwemo mahitaji msingi ya lazima, vigezo vya kutathmini uwezo wa kifedha na kitaalamu zinaweza kupatikana na wanaotaka kushiriki ***bila malipo*** kutoka kwa wavuti wetu : **http://www.irrigation.go.ke/tenders** au lango kuu la serikali la ununizi **http://www.supplier.treasury.go.ke** kuanzia **Februari 21, 2023.**

Wanaotaka kushiriki **LAZIMA** wawasilishe majina na anwani zao kwa: **purchasing@irrigation.go.ke** au **enquiries@irrigation.go.ke** kwa mawasiliano na ufafanuzi zaidi wakati wa mchakato wa utoaji tenda.

**Anwani**
**Afisa Mkuu Mtendaji/CEO**
**National Irrigation Authority (NIA)**
**Irrigation House,**
**Lenana Road, Hurlingham, Nairobi, Kenya**
**Tel: +254-20-2711380/468**
**Fax: +254-20-2722821/2711347**
**E-mail: ceo@irrigation.go.ke; purchasing@irrigation.go.ke**

**CHIEF EXECUTIVE OFFICER/CEO**
**NATIONAL IRRIGATION AUTHORITY**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

CAPITAL MARKETS AUTHORITY
Promoting the Integrity and Growth of the Capital Markets

## AJIRA YA MWEKEZAJI WA MASOKO YA MTAJI WATU WA KUJITOLEA KUTOA MAFUNZO

1) **Je, una ari ya kuihudumia jamii katika ngazi ya chini?**
2) **Je, unafahamu vipengele mbalimbali vya masoko ya mitaji nchini Kenya?**
3) **Je, una uzoefu na usimamizi wa hafla na kuuzungumzia umma, na unaweza kushughulika na vikundi vya takriban watu 30 au zaidi?**
4) **Je, wewe binafsi umewekeza, au una nia, katika hisa na dhamana zilizoorodheshwa ndani ya Soko la Kuuza Hisa la Nairobi na katika Unit Trust?**

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji (CMA) ina fursa ya kusisimua kwa watu wa kujitolea kufanya mazungumzo ya elimu ya uwekezaji yanayolenga umma kwa ujumla hasa katika ngazi ya Kaunti kwa muda wa miezi ishirini na nne (24). Lengo kuu la mpango huu ni kuongeza uelewa na ushirikishwaji katika masoko ya mitaji kwa kuwashirikisha ipasavyo walengwa mbalimbali. Hii inaendana na moja ya majukumu ya Mamlaka ya kukuza elimu ya uwekezaji na uhamasishaji wa umma Nchini kote. Kuna malipo madogo yanakayotolewa kwa kila kikao.

Ikiwa unaamini kuwa umehitimu kushiriki katika fursa hii ya kusisimua, tafadhali tuma maombi yako (upeo wa ukurasa mmoja), ambao unapaswa kuonyesha wazi ufaafu wako kwa kazi kama ilivyoainishwa hapo juu ikiambatana na muhtasari wa wasifu wako au Curriculum Vitae (ukubwa wa hadi kurasa mbili).

Maombi yanaweza kuwasilishwa kupitia nakala halisi kwa Afisa Mkuu Mtendaji, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji au kupitia barua pepe katika iepa@cma.or.ke. Maombi lazima yapokewe kabla ya tarehe **8 Machi, 2023.**

**MAMLAKA YA MASOKO YA MTAJI**
**Embankment Plaza, Orofa ya 3**
**Barabara ya Longonot, kando na Kilimanjaro Avenue, Upperhill**
**P.O Box 74800-00200, Nairobi Kenya**
**Simu: +254 20 2264400/ 2264900/ 2221910/ 2221869**
**Laini Mbadada Zisizotumia Waya: 0722 207767/020 2611464**
**Rununu: +254 722 207767**

KOMESHA COVID-19

" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"

HOMA
KIKOHOZI
KUSHINDWA KUPUMUA
MAUMIVU KOONI
KUUMWA NA KICHWA

# Ushirikiano wa Serikali, sekta ya kibinafsi kuongeza uzalishaji wa mifugo

NA CHRIS MAHANDARA (KNA)

Serikali imeshirikiana na sekta ya kibinafsi kuongeza uzalishaji wa mifugo nchin. Kupitia mradi wa kufanya ufugaji kuwa biashara Kenya (KeLCoP), mpango huu unalenga kusaidia wakulima katika mifumo ya thamani ya ufugaji wa kuku walioimarishwa, mbuzi wa maziwa, asali na nyama ya mbuzi na ya kondoo.

Mradi huo wa miaka mitano, unaofadhiliwa na Hazina ya Kimataifa ya Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Serikali ya Kenya kwa Sh9.4 bilioni unalenga kufanya uzalishaji wa mifugo kuwa biashara katika kaunti kumi kwa majaribio.

Katibu wa Idara ya Serikali ya Mifugo Harry Kimtai, alisema kwamba hatua hiyo inanuiwa kupiga jeki mapato ya familia zaidi ya 110 katika kaunti lengwa.

"Tulichagua maeneo haya manne kwa sababu ya hali ya watu masikini sehemu za mashambani ili tuweze kuongeza mapato yao," alisema. Ingawa mradi huo pia umevutia ruzuku kutoka Heifer International kwa wakulima wanaofuga nguvu ng'ombe wa maziwa, Katibu alisema serikali itashirikiana na sekta ya kibinafsi kuhusisha wakulima zaidi na kuhakikisha mradi huo umeendelezwa.

Akizungumza akiwa Kisumu kufunga warsha ya siku tano ya kuleta ushirikiano na wadau wakuu kutoka sekta ya ki-

> Tulichagua maeneo haya manne kwa sababu ya umaskini mashinani "-PS Kimtai



Katibu wa Idara ya Mifugo (PS), Harry Kimtai, ahutubia waandishi habari mjini Kisumu. Kushoto ni msimamizi wa Wakfu wa KCB, Caroline Wanjeri na Mkurugenzi Mkuu wa Kenchic, Jim Tozer (Kati). PICHA: CHRIS MAHANDARA (KNA)

binafsi, Katibu alisema kwamba ushirikiano huo unataka kutumia na kujifunza kutoka ufanisi wa sekta ya kibinafsi, kupata matokeo bora katika vita dhidi ya njaa na umasikini.

"Tumekuwa na mazungumzo na sekta ya kibinafsi kuona jinsi tunaweza kuunga mpango huu. Tumeshauriana nao kuhusu maeneo ya ushirikiano na kila mmoja wao atachukua eneo linalomvutia," alisema.

Miongoni mwa washirika, alisema ni Kenchic, Wakfu wa KCB na taasisi kadhaa za kifedha ambazo zinatarajiwa kuweka pesa katika mpango huo kusaidia wakulima wanaohusishwa katika mradi huo.

"Tunanuia kukopa kutoka utafiti mpana uliofanywa na washirika kama Kenchic kusaidia wakulima masikini sehemu za mashambani kufikia biashara," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Kenchic, Jim Tozer, alipongeza ushirikiano huo akisema utasaidia kuimarisha sekta ya ufugaji wa kuku nchini.

Kampuni hiyo ambayo imekuwa katika biashara hiyo kwa miaka 40 iliyopita, alisema, ina utafiti wa kina na idara ya huduma za nyanjani ambayo itasaidia serikali inapochukua hatua za kuongeza mapato katika mfumo wa thamani.

Kenchic pamoja na washirika, alisema, tayari inahusika na mipango ya nyumba na lishe kote nchini na akaongeza kuwa ushirikiano na serikali utasaidia vijana wengi na wanawake kujiunga na ufugaji wa kuku.

---

REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA ARDHI, KAZI ZA UMMA, UJENZI NA USTAWISHAJI WA MIJI

*IDARA YA UJENZI NA USTAWISHAJI WA MIJI*

## TANGAZO LA ZABUNI

Serikali ya Kenya kupitia Wizara ya Ardhi, Kazi za Umma, Nyumba na Ustawishaji wa Miji, Idara ya Ujenzi na Ustawishaji wa Miji, inakusudia kuwahusisha watoa huduma waliohitimu kwa huduma zifuatazo:

| NA | JINA LA MRADI | NAMBA YA ZABUNI | DHAMANA | KIWANGO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Utoaji wa Uandishi wa chini wa Bima ya Ulinzi wa Rehani ya Kikundi kwa Mpango wa Makazi ya Watumishi wa Umma na Mpango wa Uboreshaji wa Makazi duni huko Mavoko SNP. | MLPWHUD/SDHUD/CSHS/075/2022-2023 | 250,000.00 | Zabuni Wazi |
| 2. | Uandishi Bima ya Kikundi cha Bima ya Moto,Hatari Zinazohusiana kwa Mpango wa Nyumba ya Watumishi Umma na Uboreshaji wa Makazi duni katika Majengo ya Makazi ya Mavoko SNP | MLPWHUD/SDHUD/CSHS/076/2022-2023 | 250,000.00 | Zabuni Wazi |

1. Katibu katika Idara ya Ujenzi na Ustawishaji wa Miji anakaribisha zabuni zilizofungwa kwa ajili ya utoaji wa Hati ya chini ya Bima ya Kuzima Moto na Hatari Zinazohusiana kwa Hazina ya Mpango wa Makazi ya Watumishi wa Umma na Mpango wa Kuboresha Makazi duni katika Mpango wa Makazi Endelevu wa Mavoko (SNP) Housing Estate.
2. Wazabuni wanaovutiwa wanaweza kufikia hati ya zabuni kutoka kwa tovuti ya Idara www.housingandurban.go.ke au Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma (PPIP) https://tenders.go.ke ***bila malipo.*** Wazabuni wanaweza kupakua hati za zabuni kutoka kwa tovuti na wanatakiwa kutoa maelezo yao kwa kujisajili na Afisi ya Usimamizi wa Mfumo wa Usambazaji, iliyoko Ardhi House, Orofa ya 6, Wing B, 1st Ngong Avenue, wakati wa saa za kawaida za kazi. Maswali na ufafanuzi wote utumwe kupitia barua pepe kwa: procurementhousingandurban@gmail.com
3. Wazabuni watatoa taarifa ya Usalama wa Zabuni ya Dhamana ya Benki ya kiasi cha **Shilingi za Kenya Laki Mbili na Hamsini Elfu (Ksh. 250,000.00).**
4. Nyaraka zilizokamilishwa za zabuni zilizoambatanishwa katika bahasha zilizofungwa wazi na kuwekwa alama ya wazi kwa Nambari ya Zabuni na Maelezo ya Zabuni zitawasilishwa kwa anuani iliyo hapa chini au kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni lililopo Ardhi House, Orofa ya 6 (Eneo la Kuinua Lift) ili ilipokelewa mnamo au kabla ya **Jumanne, 7 Machi 2023 saa 11.00 asubuhi**. Hati nyingi zitawasilishwa na kusajiliwa katika Afisi ya Mkuu, Huduma za Usimamizi wa Mfumo wa Usambazaji katika Ardhi House, Oorofa ya 6, Mrengo B.
5. Zabuni zitafunguliwa mara moja baada ya hapo katika Ukumbi wa Mikutano wa Idara ya Ujenzi na Ustawishaji wa Miji, iliyoko Ardhi House, 6thFloor, Wing B mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria.
6. Zabuni zilizochelewa zitakataliwa.

**Mkuu wa Usimamizi wa Huduma za Usambazaji**
**Kwa: Katibu wa Wizara**
**Idara ya Ujenzi na Ustawishaji wa Miji**
**P.O. Boz 30119 -00100**
**NAIROBI**

KENYA VISION 2030

---

REPUBLIC OF KENYA

Kenya Power

## MWALIKO WA ZABUNI

Kenya Power inakaribisha zabuni kutoka kwa wazabuni wanaovutiwa kwa yafuatayo:-

| NO. | NAMBARI YA ZABUNI | MAELEZO YA ZABUNI | MWANZO WA ZABUNI | KUZURU ENEO/KIKAO | TAREHE YA KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KP1/9A.2/OT/035/22-23 | Ununuzi wa Huduma ya Kurekebisha Mizinga ya Mafuta katika Vituo vya Umeme vya Lokiriama, Banissa, Marsabit na Lodwar Nje ya Gridi | Jumanne 21.02.2023 | N/A | Jumatano 08.03.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 2. | KP3/9A/OT/02/ADMIN/22-23 | Mapendekezo ya Maduka ya Wingi na Ukarabati wa Karakana ya Mitambo ya Umeme | Jumanne 21.02.2023 | **Jumanne 28.02.2023 saa 11.00 asubuhi (Maduka ya Wingi ya KPLC)** | Ijumaa 10.03.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 3. | KP6/5C/OT/01/HRA/22-23 | Pendekezo la Ujenzi wa Ghala la Voi na Kazi Zilizounganishwa za Nje - Eneo la Pwani | Jumanne 21.02.2023 | **Alhamisi 02.03.2023 saa 10.00 a.m. (Depo ya Kenya Power - Mji mdogo wa Voi)** | Jumanne 14.03.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 4. | KP1/9A.2/OT/042/SEC/22-23 | Usambazaji na Usanidi wa Kadi za Ufikiaji wa Biometriska, Vifaa vya Mtandao na Vifuasi | Jumatano 22.02.2023 | N/A | Jumatano 15.03.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 5. | KP1/9A.2/OT/032/ICT/22-23 | Upatikanaji wa Njia Mpya za Muunganisho wa Mtandao kwa Ofisi Mpya na Zijazo | Jumatano 22.02.2023 | N/A | Jumatano 15.03.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 6. | KP5/9A/3/10/OT/03/22-23 | Construction of Embu Commercial Office, Embu Town – Mt. Kenya Region | Jumatano 22.02.2023 | Friday 10.03.2023 at 11.00 a.m. **(Embu Office)** | Jumanne 21.03.2023 saa 10.00 asubuhi |

Nyaraka za zabuni zinazoelezea mahitaji ya zabuni zilizo hapo juu zinaweza kupatikana kutoka kwa tovuti ya Kenya Power (www.kplc.co.ke) kuanzia tarehe zilizoonyeshwa hapo juu.

**MENEJA MKUU**
**MFUMO WA USAMBAZAJI NA VI-**

**www.kplc.co.ke**

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy




REPUBLIC OF KENYA

# WIZARA YA AFYA

## IMETANGAZWA TENA

## AFISA MSIMAMIZI FEDHA WA MRADI

| | |
|---|---|
| **NAMBA YA NAFASI** | **01/2022** |
| **MFUMO WA KAZI** | **KANDARASI** |
| **ANARIPOTI KWA** | **MKUU-IDARA YA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA KITAIFA YA AFYA** |
| **ENEO LA KAZI** | **NAIROBI** |

Wizara ya Afya kwa msaada wa Hazina ya Kimataifa ya Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria inalenga kuajiri mtu mwenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya Afisa Fedha wa kitengo cha Global Fund katika Idara ya Uimarishaji wa Mifumo ya Afya ya Taifa kwa Mkataba.

Afisa wa Fedha ataratibu na kutekeleza miamala na shughuli za kifedha kwa shughuli za ruzuku ya Global Fund.

Watu wanaovutiwa na waliohitimu wanaombwa kuwasilisha maombi ya maandishi pamoja na wasifu wa kina (CV), nakala za Kitambulisho cha Taifa, vyeti vya masomo na taaluma na stakabadhi nyingine husika kwa anwani ifuatayo:

**Katibu,**
**Wizara ya Afya,**
**P.O. Box 30016-00100,**
**NAIROBI.**

Maombi yanaweza pia kutumwa kwa barua pepe kupitia: **directorhrmoh@gmail.com** au kuwasilishwa kwa mkono kwa Wizara ya Afya, Afya House, Orofa ya 3, Chumba 312 (Masjala) kabla ya tarehe **7 Machi, 2023 saa 5.00 jioni (Saa za Afrika Mashariki).**

### Mahitaji ya Uteuzi

Wagombea wanaotaka kuomba nafasi hiyo hapo juu lazima wawe na yafuatayo:

i. Shahada ya digrii katika somo lolote kati ya yafuatayo: Biashara (Chaguo la Fedha), Uchumi, Usimamizi wa Biashara, Fedha na sifa nyingine zozote zinazohusiana na biashara kutoka kwa taasisi inayotambuliwa;
ii. Mhasibu wa Umma aliyeidhinishwa - CPA (K);
iii. Mwanachama wa ICPAK na mwenye hadhi nzuri;
iv. Angalau uzoefu wa miaka 3 wa kufanya kazi katika mradi unaofadhiliwa na wafadhili;
v. Ujuzi wa kisasa wa uhasibu wa kompyuta kama vile Quick books, Pastel, SAGE na Navision, miongoni mwa zingine,

### Uwezo wa Msingi

i. Ujuzi wa mipamgo ya Serikali ya Kenya, kupanga bajeti na taratibu za usimamizi wa fedha;
ii. Ujuzi wa mpangilio wa mfumo wa utoaji wa huduma za afya nchini Kenya, ikijumuisha mfumo wa afya uliogatuliwa;
iii. Onyesha uwezo na kujitolea kwa kazi ya pamoja na uratibu na washirika wengi;
iv. Uwezo wa kufanya kazi ndani ya muda uliowekwa;
v. Mwenye ari na ubunifu;

### Wajibu na Majukumu

Wajibu na majukumu ya mwenye wadhifa huo yatajumuisha:
i. Kushiriki katika uundaji wa bajeti za Global Fund wakati wa maombi ya ufadhili, utayarishaji wa ruzuku na ugawaji upya;
ii. Kuandaa bajeti za kila mwaka za Globa Fundl;
iii. Kuhakikisha kuwa bajeti za Global Fund zimenakiliwa katika makadirio yaliyochapishwa ya GoK/MoH;
iv. Kuandaa mgao wa fedha dhidi ya shughuli, kwa malipo yote yaliyopokelewa kutoka kwa Mpokeaji Mkuu;
v. Kusimamia na kutoa mafunzo kwa wahasibu katika kitengo kwa ajili ya utekelezaji bora wa chombo cha Ufuatiliaji wa Fedha iliyoandaliwa na Mpokeaji Mkuu;
vi. Kutumia zana ya ufuatiliaji wa Fedha kufuatilia gharama dhidi ya shughuli ambazo ulipaji ulifanywa;
vii. Kuhakikisha matumizi yote ya ruzuku yanafanyika kwa kuzingatia mahitaji na taratibu za kifedha za GoK na Global Fund;
viii. Kuweka rekodi ya malipo yote kwa Mpokeaji Mdogo na gharama zinazohusiana;
ix. Kuhakiki ankara zote zilizowasilishwa na wakala wa manunuzi ili kuhakikisha kuwa zinazingatia Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Umma na makubaliano kati ya Mpokeaji Mkuu na wakala wa Manunuzi;
x. Kutayarisha ripoti za fedha za mara kwa mara kuhusu shughuli za ruzuku ya Global Fund kama inavyotakiwa na Mpokeaji Mkuu;
Xi. Kuhakikisha kuwa maswali kuhusu usimamizi wa fedha na ripoti za fedha za mpokeaji Mdogo kama yanavyoweza kuulizwa na Wakala wa Hazina wa Ndani au sekretarieti ya Mfuko wa Kimataifa yanashughulikiwa Mara moja;
xii. Kutayarisha makadirio ya fedha taslimu kwa ajili ya ruzuku ya mpokeaji Mdogo; na
xiii. Kutekeleza majukumu mengine yoyote kama itakavyoagizwa na Mkuu, Idara ya Uimarishaji wa Mifumo ya Kitaifa ya Afya mara kwa mara.

### Malipo

Mgombea atakayefaulu atalipwa malipo mazuri

### Mambo Muhimu ya Kuzingatia

i. Mwombaji anapaswa kutoa maelezo yote yaliyoombwa katika tangazo;
ii. Ni kosa kuingiza taarifa zisizo sahihi katika maombi;
iii. Maelezo ya vyeti vya kitaaluma na kitaaluma ambayo hayatakuwa yametolewa kufikia kufungwa kwa tangazo hayatajumuishwa;
iv. Tutawasiliana tu na wagombea watakaoorodheshwa;
v. Ombi la yeyote atakayepatikana akidanganya litafutiliwa mbali;
vi. Waombaji walioorodheshwa watahitajika kutoa hati asili za Kitambulisho chao cha Taifa, vyeti vya kitaaluma na nakala wakati wa usaili;
vii. Ni kosa la jinai kuwasilisha vyeti/nyaraka feki;
viii. Maafisa wanaohudumu watahitajika kutoa barua ya awali ya uteuzi kwa wadhifa wao wa sasa wakati wa mahojiano.

Wizara ya Afya imejitolea kutekeleza masharti ya Katiba - Sura ya 232 (1) kuhusu ushindani wa haki na sifa, uwakilishi wa jamii mbalimbali za Wakenya na kutoa fursa sawa za ajira kwa wanaume na wanawake, watu wa makabila yote na watu wenye ulemavu, kwa hivyo, watu wenye ulemavu, waliotengwa na walio wachache wanahimizwa kutuma maombi.

**KATIBU WA WIZARA**

KENYA VISION 2030

---

REPUBLIC OF KENYA

Kenya Power

## Taasisi ya Mafunzo ya Nishati & Utafiti

## KOZI ZA DIPLOMA NA VYETI – Undikishaji wa MEI 2023

Taasisi ya Mafunzo ya Nishati na Utafiti (IESR) ni Taasisi iliyoidhinishwa ya Elimu ya Kiufundi ya Viwanda na Ufundi nchini Kenya chini ya Sheria ya TVET 2013 na Taasisi ya Mafunzo ya Viwanda iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Mafunzo ya Viwanda Sura ya 237 ya 2011. Kozi zetu zinachunguzwa na Baraza la Kitaifa la Mitihani (KNEC). IESR inamilikiwa kibinafsi na Kenya Power na pia imesajiliwa kama Taasisi ya Utafiti. IESR inakaribisha maombi ya kozi zifuatazo kwa uandikishaji wa Mei 2023. Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ni **Ijumaa, tarehe 10 Machi 2023.**

| NA. | JINA LA KOZI | SHARTI | MUDA NA ADA YA MASOMO |
|---|---|---|---|
| | **KOZI ZA DIPLOMA** | | |
| 1. | **Diploma ya Uhandisi wa Umeme na Elektroniki (Chaguo la Umeme/Elektroniki) Sehemu ya 1 (KNEC) – Mchana/Jioni** | Kiwango cha chini cha KCSE wastani alama ya C- (Minus) na D+ (Plus) katika Kiingereza, Hisabati na Fizikia/ Sayansi Asilia | **Miaka 3 ya mihula 7 darasani na mihula 2 ya masomo ya nyanjani. Karo ya Muhula wa Kwanza KShs.38,900/=** |
| 2. | **Diploma ya Uhandisi wa Umeme na Elektroniki (Chaguo la Umeme) Sehemu ya II (KNEC) - Mchana/ Jioni** | **Diploma ya Umeme na Uhandisi wa Kielektroniki - (Chaguo la Umeme) Sehemu ya I (KNEC) AU Cheti cha Ufundi katika Umeme na Kielektroniki Uhandisi - (Chaguo la Umeme)** | **Miaka 2 ya mihula 5 darasani na mihula 2 ya masomo ya nyanjani Karo ya Muhula wa Kwanza KShs.45,900/=** |
| 3. | **Diploma ya Uhandisi Mitambo Chaguo la Mitambo Sehemu 1 (KNEC) - MCHANA** | Kiwango cha chini cha KCSE wastani cha Alama ya C- (Minus) na D+ (pamoja na) katika Kiingereza, Hisabati na Fizikia/Sayansi Asilia | **Miaka 3 ya mihula 7 darasani na mihula 2 ya nyanjani. Karo ya Muhula wa Kwanza KShs.38, 900/=** |
| 4. | **Diploma ya Uhandisi wa Magari MCHANA Sehemu I** | Kiwango cha chini cha KCSE wastani Alama ya C- (Minus) na D+ (pamoja na) katika Kiingereza, Hisabati na Fizikia/Sayansi Asilia | **Miaka 3 ya mihula 7 darasani na mihula 2 ya nyanjani. Karo ya Muhula wa Kwanza KShs.38,900/** |
| 5. | **Diploma ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano MCHANA Sehemu i** | Kiwango cha chini cha KCSE wastani Alama ya C- (Minus) na D+ (pamoja na) katika Kiingereza na Hisabati | **Miaka 3 ya mihula 7 darasani na mihula 2 ya nyanjani. Karo ya Muhula wa Kwanza KShs.38,900/** |
| | **KOZI ZA VYETI** | | |
| 6. | **Cheti cha Ufundi katika Uhandisi wa Umeme na Elektroniki (Chaguo la Umeme) (KNEC) – Mchana/Jioni** | Kiwango cha Chini cha KCSE Wastani Alama ya D (plain), na D (plain) katika Hisabati, Kiingereza na Fizikia/Sayansi Asilia | **Miaka 2 ya mihula 5 darasani na muhula 1 wa nyanjani. Karo ya Muhula wa Kwanza KShs.38,900/=** |
| 7. | **Ufundi katika Uhandisi wa Magari MCHANA** | Kiwango cha Chini cha KCSE Wastani Alama ya D (plain) pamoja na D (plain) katika Kiingereza, Hisabati & Fizikia /Sayansi Asilia | **Miaka 2 ya mihula 7 darasani na mihula 2 nyanjani. Karo ya Muhula wa Kwanza KShs.38,900/=** |
| 8. | **Ufundi katika Uhandisi wa Mitambo (Chaguo la Uzalishaji) MCHANA** | Kiwango cha Chini cha KCSE Wastani Alama ya D (plain) pamoja na D (plain) katika Kiingereza, Hisabati & Fizikia /Sayansi Asilia | **Miaka 2 ya mihula 7 darasani na mihula 2 nyanjani. Karo ya Muhula wa Kwanza KShs.38,900/-** |
| 9. | **Cheti cha Ufundi katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (KNEC) - MCHANA** | Minimum KCSE Mean Grade of D (Plain) with D (Plain) in Mathematics, English | 2 years of 5 terms in class and 1 term of attachment. Term one Fees **KShs.38,900/=** |

Alifichua kwamba Lamu itapokea jumula ya Sh500 milioni wakati mradi wa miaka mitano wa Sh10 bilioni wa KEMSFED utaanzishwa kikamilifu. Ruzuku za KEMSFED zinatekeleza chini ya Mpango wa Kuinua Maisha ya Jamii za Pwani ambao Lamu itapokea Sh49 milioni katika awamu ya kwanza. "Kumekuwa na shinikizo nyingi hasa kutoka kwa serikali yangu, pesa hizo zitokewe kwa wakati, tangu nilipoteuliwa mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi wa Baharini ya Baraza la Magavana," aliongeza. Vile vile aliongeza kuwa mipango inaendelea kujenga kiwanda cha samaki, kiwanda cha barafu na eneo la kutayarisha samaki katika mji wa Mokowe katika hatua aliyosema itabuni nafasi za ajira.

Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Baharini wa kaunti hiyo Faiz Fankupi aliyezungumza katika hafla hiyo alihakikishia makundi yanayohusika kujitolea kwa kaunti kuyasaidia kufanya sekta ya uvuvi kuwa ya kisasa.

Alisema kwamba ruzuku hizo zinanuiwa kufadhili shughuli za maisha kusaidia wavuvi kupata njia za kujikimu kimaisha kama njia moja ya kupunguza kutegemea uvuvi huku samaki wakipungua kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Fankupi aliongeza kuwa serikali ya kaunti inaendeleza mchakato wa kupata hati za kumiliki ardhi za maeneo yote ya kutua samaki katika kaunti ya Lamu ili kuzuia yasinyakuliwe.


REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO YA UCHUMI

### MWALIKO WA ZABUNI

### ZABUNI YA KUKODISHA MAGARI MPANGO AWAMU YA VII

### NAMBA YA ZABUNI. TNT/017/2022-2023

WIzara ya Fedha inakaribisha Zabuni zilizofungwa kutoka kwa Watengenezaji Halisi wa Magari, Wauzaji wa Magari, Makampuni ya Kukodisha na Mashirika Yanayokusudiwa kwa Utoaji wa magari 1,652 kwa ajili ya Utawala wa Serikali ya Kitaifa, Huduma ya Kitaifa ya Polisi, Huduma za Magereza ya Kenya na MDA nyinginezo za Mpango wa Kukodisha Magari Awamu ya VII.

**Kongamano la Lazima la Zabuni** ya Mapema litafanyika pamoja na Wazabuni wanaovutiwa mnamo **Jumatano tarehe 1 Machi, 2023 saa 1000, saa za Kenya** kupitia mkutano wa mtandaoni. Mialiko itatumwa kwa wazabuni wote wanaovutiwa ambao watawasilisha barua pepe zao kwa procurement@treasury.go.ke kabla ya **Saa 1000, Saa za Kenya** mnamo **Jumatano tarehe 1 Machi, 2023.**

Wazabuni watawasilisha mapendekezo ya **Kiufundi** na **Fedha** katika bahasha tofauti.

Seti kamili ya Hati za Zabuni inaweza kupakuliwa na wagombeaji wanaovutiwa na wanaostahiki ***Bila Malipo*** katika http://treasury.go.ke au www.tenders.go.ke. Wale wanaopakua hati kutoka kwa wavuti lazima wapeleke maelezo yao mara moja ili kurekodiwa na ufafanuzi wowote zaidi na nyongeza kwa procurement@treasury.go.ke.

Nyaraka za Zabuni zilizokamilishwa, ***"Halisi"*** na ***"Nakala"***, zilizoambatanishwa katika bahasha iliyofungwa na kuwekewa Nambari ya Zabuni, zitatumwa kwa: -

**Katibu,**
**Wizara ya Fedha,**
**P.O. Box 30007 00100**
**Nairobi**

na kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni lililotolewa katika **Wizara ya Fedha, Jengo la Treasury, Orofa ya 6, Barabara ya Harambee, Nairobi,** ili ipokewe mnamo au kabla ya hapo **Jumatano tarehe 8 Machi, 2023 saa 11.00 asubuhi saa za Kenya.**
Hati zote za Zabuni lazima ziwe na zimepangwa vizuri na kuandikwa kurasa.

Zabuni zote lazima ziambatane na Dhamana ya Benki ya **Shilingi Milioni Tano Pekee (Ksh. 5,000,000.00)** kutoka kwa Benki Inayoaminika nchini Kenya halali kwa siku 30 zaidi ya muda wa Uhalali wa Zabuni.

Zabuni zitafunguliwa mara moja mbele ya Wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria ufunguzi huo katika **Wizara ya Fedha, Jengo la Treasury, Barabara ya Harambee, Nairobi, Orofa ya 6, Chumba cha Mikutano nambari 603 siku ya Jumatano tarehe 8 Machi, 2023 saa 11.00 asubuhi kwa Saa za Kenya.**

**MKUU, USIMAMIZI WA HUDUMA ZA USAMBAZAJI**
**KWA: KATIBU/ WIZARA YA FEDHA**

KENYA VISION 2030



REPUBLIC OF KENYA

## SALARIES AND REMUNERATION COMMISSION

SRC Salaries & Remuneration Commission

### PENDEKEZO LA KUTATHMINI MARUPURUPU YA KUTOFANYA KAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

### MWALIKO WA KUTUMA MEMORANDA

Salaries and Remuneration Commission (SRC) imeanzishwa chini ya Sheria 230 ya Katiba ya Kenya, 2010, a) kuweka na kutathmini mara kwa mara mshahara na marupurupu ya Maafisa wa Serikali, na b), kushauri serikali za kaunti na ile ya kitaifa kuhusu marupurupu na mishahara ya watumishi wa umma.

SRC, inapotathmini, kuamua na kushauri kuhusu mishahar na marupurupu yanayofaa katika utumishi wa umma, huwa inaongozwa na kanuni zilizoratibiwa kwenye Kifungu 230(5) cha Katiba, na Sehemu ya 12 ya Sheria ya SRC, 2011.
Kwa kuzingatia wajibu wa SRC, kama ulivyofafanuliwa kwenye Kifungu 230(4) cha Katiba, na sambamba na kanuni zilizowekwa kwenye Kifungu 230(5) cha Katiba, na Sehemu ya 12 ya Sheria ya SRC, 2011, SRC inapendeleza kutathmini Marupurupu ya Kutofanya Kazi katika Utumishi wa Umma.

Hivyo basi, kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Katiba, SRC inaalika washikadau na umma kwa jumla kuwasilisha memoranda kuhusu tathmini hiyo ya Marupurupu ya Kutofanya Kazi katika Utumishi wa Umma.
Mapendekezo hayo yanapasa kutumwa kwa Katibu wa Tume/CEO na nakala kutumwa kwa njia ya baruapepe kwa info@src.go.ke na allowances@src.go.ke, ili kupokelewa mnamo au kabla ya **Jumanne, Machi 7, 2023**.

Pendekezo kuhusu marupurupu hayo laweza kupatikana kwenye mtandao wa SRC linki:
***https://src.go.ke/download/proposal-to-review-non-practice-allowance-in-the-public-service/***

### NOTISI YA TENDA

Tume inaalika wanaohitimu kushiriki tenda zifuatazo: -

| No. | Marejeo ya tenda | Maelezo ya Tenda | Washiriki | Bondi | Siku ya Mwisho |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SRC/OT/44/2022- 2023 | UTOAJI WA HUDUMA ZA FUNDI BOMBA NA FUNDI UMEME | WAZI | N/A | Machi 8, 2023 |
| 2. | SRC/OT/45/2022-2023 | UTOAJI HUDUMA ZA TEKSI | WAZI | N/A | Machi 8, 2023 |

Wale waliohitimu wanaweza kupata stakabadhi ya tenda kutoka kwa mtandao wa SRC www.src.go.ke au Public Procurement Information Portal (www.tenders.go.ke) bila malipo.

Stakabadhi zilizojazwa zinapasa kuwekwa ndani ya Sanduku la Tenda katika lango kuu la afisi za Salaries and Remuneration Commission, Ghorofa ya 6, Williamson House, Nairobi, au kutumwa kwa

**Katibu wa Tume**
**Salaries and Remuneration Commission**
**S.LP 43126-00100 NAIROBI**

Ili kupokelewa mnamo au kabla ya tarehe ya mwisho kama ilivyoelezwa hapo juu.
Tenda itafunguliwa papo hapo katika chumba cha mikutano cha SRC kwenye ghorofa ya 6, Williamson House, mbele ya wale waliotuma maombi ambao wangependa kuhudhuria.

**KATIBU WA TUME**

https://www.src.go.ke/ Salaries and Remuneration Commission @SRCKE @srckenya




" Virusi **havitembei**, watu huvisambaza, tukiacha **kutembea**, virusi vitakufa"




# Serikali yaidhinisha mkakati wa kitaifa wa Uchumi wa Baharini

**NA ERASTUS GICHOHI NA MABEL KEYA SHIKUKU (KNA)**

Wizara ya Madini na Uchumi wa Baharini na Masuala ya Ubaharia kwa ushirikiano na Mamlaka ya Ushirikiano wa serikali na Maendeleo (IGAD), imeidhinisha Mkakati wa miaka mitano wa uchumi wa baharini kusaidia nchi kuafikia uwezo kamili wa rasilmali zake za baharini. Waziri Salim Mvurya alisema kwamba kutayarishwa kwa Mkakati huo kumejiri wakati unaofaa na kutusaidia matumizi ya rasilmali za baharini ambazo zina uwezo mkubwa katika kusaidia kujenga uchumi na kubuni ajira.

Kwa wakati huu tunatumia asilimia moja pekee ya uwezo wa uchumi wa baharini, ambao ni bahari, maziwa na mito ambazo ziko na uwezo mkubwa wa kubadilisha uchumi wa nchi," akasema Mvurya. Akizungumza katika zoezi la uhalalishaji Naivasha, Waziri alisema kwamba Kenya imeidhinisha Mkakati wa Uchumi wa Baharini ambao ulibuniwa na nchi wanachama wa IGAD mwaka wa 2018 na utazinduliwa baadaye.

Alisema kwamba Wizara itaunda sera, miswada na kanuni zitakazokuwa sheria zinazohitajika kusaidia utekelezaji wa mkakati huo



**Waziri wa Madini, Uchumi Baharini na Maswala ya Bahari Salim Mvurya [kulia] azungumza na gavana wa Lamu na mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi Baharini katika Baraza a Magavana Issa Timamy kwenye kongamano la kuidhinisha Mkakati wa Uchumi Baharini Kenya mjini Naivasha.**

Wizara yangu imetambua zaidi ya Vitengo 400 vya Usimamizi wa Fuo kote nchini ambavyo vitabadilishwa kuwa Vyama vya ushirika kufikia Juni mwaka huu kuviwezesha kupata mikopo ya kifedha na kuzibadilisha kuwa biashara," alisema Waziri.

Mvurya alisisitiza kuwa serikali itaanzisha maeneo ya kutua samaki katika sehemu zilizotengwa na kuyaweka miundomsingi muhimu kama vyumba vya baridi vya uhifadhi, vitengo vya uongezaji thamani na kuviunganisha na soko.

> Kwa sasa tunatumia asilimia 8 tu ya manufaa ya uchumi baharini," Waziri

"Hivi karibuni tutajenga mradi wa Sh1 bilioni Kisumu utakaotoa zaidi ya samaki wadogo wa kufugwa zaidi ya milioni Saba kuhudumia maziwa ya humu nchini na zaidi ya vidinbwi 2000 vya samaki kote nchini," alisema Mvurya.

Aliongeza kuwa wizara yake imehusisha Wizara ya Ulinzi kuinua ufuatiliaji katika rasilmali za baharini kutatua visa haramu vinavyozidi kuongezeka katika bahari kuu

Kulingana na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi Baharini ya Baraza la Magavana (COG) Issa Timamy, mkakati huo utahakikisha rasilmali za uchumi wa baharini zinatumiwa kikamilifu ili kuunda nafasi za ajira na kuimarisha maisha

Timamy, ambaye ni gavana wa Lamu alisema kwamba wameshirikiana na Serikali ya Kitaifa kuanzisha maeneo ya kutua samaki Lamu ili kusaidia shughuli za uvuvi katika Bahari Hindi.

Mwakilishi wa IGAD Dkt Fatuma Adan alisema kwamba shirika hilo la kikanda litasaidia serikali kuafikia uwezo wa rasilmali za baharini.

Dkt Adan alisema kwamba Kenya ni miongoni mwa nchi chache ambazo zimenufaika na ufadhili kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kukuza mchango wa uchumi wa baharini kwa pato la nchi.

Akizungumza katika hafla hiyo, mbunge wa Njoro Charity Kathambi Chepkwony, ambaye ni mwanachama wa kamati ya Bunge kuhusu Uchumi wa Baharini alisema Bunge itaunda sheria zinazohitajika kusaidia utekelezaji wa mkakati huo.

# Wanasayansi waimarisha utafiti wa nazi kuinua sekta

**NA RIPOTA WA MYGOV**

Wanasayansi wamezidisha utafiti kuhusu ubunifu wa kitekinolojia ili kupata manufaa zaidi kutoka kwa sekta ndogo ya nazi iliyo na uwezo unaokadiriwa kuwa Sh25 bilioni.

Hatua hizo katika utengenezaji inayolenga kunufaisha biashara ndogo na za kati zinatekelezwa chini ya mapango wa utafiti unaoongozwa na Chuo Kikuu cha Kilimo na Tekinolojia cha Jomo Kenyatta (JKUAT), unaohusisha ushirikiano wa taasisi na idara tofauti unanuiwa kuimarishja ushindani wa Kenya katika utengenezaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani, hasa nazi.

Akihutubia wanafunzi wa uzamili baada yao kuwasilisha mradi wa utafiti, na wanachama wa mradi huo katika JKUAT, Prof. Bernard Ikua, Naibu Makamu Chansela anayesimamia Usimamizi na Fedha katika taasisi hiyo alihimiza wanafunzi hao "kutia bidii ili kupata ufanisi ambao utaimarisha mfumo wa thamani wa nazi Kenya na kote ulimwenguni."

Prof. Ikua alihimiza wanafunzi hao kuzingatia usimamizi wa muda na kukijita katika utafiti wao ili kukamilisha masomo yao ndani ya muda uliowekwa.

Akisema kwamba utafiti huo unahusu mambo mengi, alihimiza wanafunzi " kujifunza kutangamana ili kuinua matokeo yanayotarajiwa na kuimarisha sekta ndogo ya nazi."

Wanafunzi hao wa uzamili wamenufaika na ruzuku ya utafiti kutoka Mwenyekiti wa Utafiti wa Utengenezaji kutoka kwa Kituo cha Kimataifa cha Maendeleo ya Utafiti (ICDRC) cha Canada kupitia Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Tekinolojia na Ubunifu (NACOSTI).

Walitoa mawasilisho yao katika Nyanja za vifaa na mashine, urembo na bidhaa za urembo, kawi na viumbe hai, na uchumi jamii. Nyanja zingine zilikuwa ni chakula na vinywaji, nguo na faiba.

Miradi hiyo ya utafiti itatumiwa kwa muundo na utengenezaji wa mashine, tekinolojia, na ufahamu wa utengenezaji unaolenga kutatua mapengo katika mfumo wa uongezaji thamani wa nazi katika ukanda wa Pwani ambako mumea huo unapandwa lakini haujapatiwa umakinivu unaotosha kuutumia vyema kutokana na changamoto.

# Waziri apongeza wakuu TVET kwa mageuzi yaliyosisimua sekta ya elimu

**NA HAMDI MOHAMUD**

Waziri wa Elimu, Ezekiel Machogu amepongeza mabadiliko yaliyoanzishwa katika sekta ya TVET miaka 15 iliyopita akisema yamebadilisha elimu ya kiufundi kwa miundomsingi na vifaa vya kisasa vya kutoa mafunzo.

Machogu alikuwa akizungumza katika Chuo cha Mafunzo ya Elimu ya Kiufundi cha Kenya katika warsha ya Mafunzo na Wakuu wa Taasisi za Kiufundi Kenya (KATTI) na mameneja wa kaunti wa Elimu na Mafunzo Anuai na Wakurugenzi wa Kaunti wa TVET kuhusu usimamizi bora wa taasisi hizo.

Waziri alihimiza wakuu wa taasisi hizo na wakurugenzi wa kaunti kuunda mifumo inayovutia umma kukumbatia TVET kama njia ya wanafunzi kuafikia ndoto zao za ajira kuanzia



**Waziri wa Elimu, Ezekiel Machogu (Kati) na Katibu wa SDTVET Dkt. Esther Muoria (kulia) ahutubia waandishi habari katika Kenya School of TVET, Nairobi.** PICHA: SHEILA NJOKI WANJOHI

ufundi hadi viwango vya uzamifu.

Alisema kwamba mtaala wa Elimu wa Utendaji na Umilisi na Mafunzo

(CBET) unanuiwa kutoa ujuzi mahususi na utendaji unaolandana na mahitaji ya kazi na hivyo basi kuna haja ya kutafuta mbinue za kumpiga msasa mtaala uliopo wa CBET ili uweze kutimiza mahitaji ya kazi na viwango vya kimataifa.

Waziri alisema kwamba mojawapo wa sera zinazohitaji umakini wa dharura ni uunganishaji na viwanda na akahimiza wataalamu kunyoosha mfumo kazi wa sera unaotayarishwa kuhusu uunganishaji ili sheria husika iweze kushughulikiwa.

# Kaunti yafanya ukusanyaji data za maabara kuwa dijitali kuboresha huduma

**NA ESTHER MWANGI (KNA)**

Serikali ya kaunti ya Nakuru itafanya mifumo yake ya usimamizi wa habari za maabara kuwa wa kujiendesha ili kusaidia kutatua changamoto za ukosefu wa usalama wa data na kuharibika kwa stakabadhi.

Gavana Susan Kihika alisema kwamba wanatafuta mfumo wa kisasa ambao sehemu zake kuu zitakuwa ni mtiririko wa kazi na kufuatilia data, muundo unaoweza kubadilishwa, kubadilisha data, kusaka data, kuchanganua data na kitabu za kielektroniki cha maabada (ELN).

Kihika alisema kwamba mifumo bora ya usimamizi wa maabara inarahisisha uwekaji wa rekodi, ufuatiliaji na kutoa ripoti, ambako kutasaidia kuondoa hatari za makosa ya binadamu na kuimarisha muda unaochukuliwa kutoa huduma.

"Tunatarajia kuwa na jukwaa litakalokuwa suluhu linalofanya kazi haraka na kuwezesha mawasiliano kati ya wanayasansi, wafanyabiashara, maabara na umma," alisema.

Mfumo huo wa kujiendesha, kulingana na Gavana, hautapunguza haja ya kutumia mikono kuweka data tu lakini pia utapunguza vizingiti na kunyoosha kazi ndani ya idara ya afya.

Akisisitiza ahadi yake ya kuacha kumbukumbu katika sekta ya afya, Kihika alisema kwamba amepatia kipaumbele uimarishaji wa vituo vya afya ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma nafuu na bora kwa watu wa Nakuru. Alihakikishia wakazi kwamba timu yake, kupitia ushirikiano wa sekta ya umma na ya kibinafsi, itaboresha vifaa vya kutambua magonjwa katika vituo vyote vya afya katika kaunti hiyo. Kihika alisema kwamba kuboresha hospitali za zamani na kujenga hospitali mpya za kaunti ndogo kutaokoa wakazi na shida ya kusafiri hadi hospitali ya rufaa ya kaunti ya Nakuru kwa huduma spesheli kama upasuaji.

Gavana alitangaza kuwa serikali yale inatayarisha ushirikiano kadhaa wa kimkakati kuwapa wakazi upatikanaji nafuu wa matibabu kupitia huduma za matibabu za video.

Akizungumza katika ofisi yake katika mkutano na ujumbe kutoka ElsMed Healthcare, Gavana alisema ubunifu wa huduma za afya ulimwenguni, matumizi ya tekinolojia ya mawasiliano, zimepunguza ushauri wa moja kwa moja wa daktari na mgonjwa.






# Waziri Owalo azindua maandalizi ya mkutano wa Connected Kenya 2023

**NA RACHAEL KILONZO (PCO)**

Waziri wa Habari Eliud Owalo, amepongeza wawekezaji katika sekta ya ICT Kenya kwa kuwa washirika wa serikali katika kuunda muundomsingi ya mabadiliko na kuanzisha tekinolojia dijitali kwa miaka mingi.

Akizungumza jijini Nairobi alipoongoza uzinduzi rasmi wa maandalizi ya kongamano la mwaka huu la Connect Kenya, Owalo alisema kwamba ushirikiano huo umesaidia kufanya Kenya kuwa kituo kinachoongoza cha ICT barani Afrika.

“Niko na furaha kujiunga nanyi katika hafla hii ya staftahi ya kongamano hili la Connected Kenya 2023. Ni jambo nzuri kwa serikali kubadilishana mawazo na wadau muhimu, kupitia mikutano kama huu,” alisema.


“Sote tunataka kufaulu katika juhudi hizi. Kwa pamoja tunataka kupata suluhu ya changamoto zinazotukumba. Tunazikabili pamoja na kutembea hadi siku zijazo tukiwa na imani zaidi,” Waziri Owalo alisema.

Waziri alisema kwamba ushirikiano wenye nguvu umefanya kongamano la kioa mwaka la Connected Kenya kukua kutoka mkutano mdogo mwaka wa 2009 hadi kongamano kubwa la ulimwengu.

Alisema kwamba kongamano hilo limekuwa likitoa mawazo mazuri ya ICT na kutoa suluhu kwa changamoto zinazoibuka kila wakati katika sekta hiyo ambayo Kenya imekuwa mdau mkubwa ulimwenguni.

“Kwa sababu ya mfumo mkubwa wa dijitali unaosaidiwa na mfumo kazi wetu wa uwezeshaji wa kisheria, uthibiti na sera, Kenya imekuwa makao yanayopendwa na kampuni kubwa za kimataifa za tekinolojia,” Bw Owalo aliambia hadhira wakiwemo maafisa wakuu wa kampuni kubwa katika sekta ya ICT.

> Tunasaka na kupata kwa pamoja changamoto zinazotukumba" -Owalo



Eliud Owalo

Zaidi ya kusaidia Kenya kuharakisha maendeleo ya muundomsingi wake wa ICT, Bw Owalo alishukuru washirika hao kwa kutoa nafasi za ajira kwa vijana wa Kenya, na pia kwa kufungua nafasi za kibiashara za kujiajiri.

Kuhusu kuanzishwa kwa Mpango Mkuu wa Dijitali unaoendelea, Bw Owalo alisema kwamba serikali inathamini sana ICT, ambayo Kenya Kwanza imetambua kama mojawapo ya maeneo ya kutilia mkazo. Alihimiza sekta ya kibinafsi kuhusika zaidi katika miradi inayotekelezwa, ukiwemo kufanya huduma za serikali kuwa za dijitali.

“Mpango huo unaendelea vyema. Wakenya kote nchini sasa wanaweza kupata huduma za serikali kupitia tovuti ya e-citizen au katika vituo vya Huduma.

Jukwaa hizi mbili ni matunda ya Kongamano la Connected na ahadi kutoka mikutano yetu ya awali,” alisema Waziri Owalo.

Siku zijazo, Bw Owalo alisema Wizara yake itajitahidi kupanua ushirikiano na wadau katika sekta ya ICT, kama washirika katika utekelezaji wa mpango mkuu wa dijitali wa nchi.

“Ninawatakia majadiliano mazuri na ninatazamia kongamano la Connect 2023 mwezi Aprili. Kama viongozi katika sekta hiyo, nyinyi ndio viongozi wa mawazo,"alisema.

# Kaunti yahusisha huduma za TB maeneo ya kazi kupunguza maambukizi

**NA ESTHER MWANGI (KNA)**

Serikali y kaunti ya Nakuru imeanzisha mpango wa kuhusisha huduma za Kifua Kikuu (TB) katika mipango ya afya maeneo ya kazi kusaidia kupunguza kuenea kwa ugonjwa huo.

Waziri wa Afya wa Kaunti hiyo Bi Jacqueline Osoro, alisema mpango huo unalenga kuhusisha maeneo ya kazi katika uzuiaji na matibabu ya TB. Osoro alieleza kwamba timu za usimamizi wa afya za kaunti ndogo na washirikishi wa TB na kifafa zitashirikiana kwa karibu na mradi wa Tuberculosis Accelerated Response and Care (TB ARC11) kuhusisha usimamizi na uzuiaji wa TB katika maeneo ya kazi na taasisi za masomo katka kaunti hiyo. Waziri huyo wa kaunti alisisitiza umuhimu wa kupimwa TB kila wakati katika maeneo ya kazi, ikiwemo miongoni mwa wahudumu wa afya,akisema hii itasaidia kuzuia usambazaji wa TB na matibabu.

Alihimiza wafanya kazi wa afya kuwa mstari wa mbele kuongoza kwa mfano, kwa kupimwa TB, kusaidia kujenga Imani miongoni mwa jamii kuhusu umuhimu wa kupimwa TB na kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo.

Afisa Mkuu wa Huduma za Matibabu wa Kaunti hiyo Dkt John Murima, alihimiza wahudumu wa afya kutumia wahudumu wa kujitolea wa afya wa kijamii kuwasaidia kupunguza maambukizi ya TB katika jamii.

Dkt Murima aliambia wafanyakazi wa afya katika kaunti ndogo zote 11 kuwa kwenye mstari wa mbele katika kampeni ya kupima na kuzuia, kupitia uhamasishaji mashinani.

Mradi wa TB ARC11 unaotumia ujuzi wa Kenya na ufahamu kupunguza pakubwa mzigo wa TB nchini Kenya, uliundwa na serikali ya Amerika kwa ushirikiano na wataalam wa afya wa Serikali.


KETRACO
Kenya Electricity Transmission Company Limited
"Building a World Class National Grid"

## TENDER NOTICE

The Kenya Electricity Transmission Company Limited (KETRACO) is a State Corporation wholly owned by the Government of Kenya. The Mandate of the Company is to plan, design, construct, own, operate and maintain high voltage electricity transmission grid and regional power interconnectors.

KETRACO invites bids from all interested and eligible firms for the following.

| S/no | Tender Description | Tender Reference Number | Closing Date |
|---|---|---|---|
| 1. | Provision of Helicopter Maintenance Services | KETRACO-PT-003-2023 | 1st March, 2023 at 10.00 am EAT |
| 2. | Supply & Delivery of Air Conditioning Replacement Units and AC Consumables | KETRACO-PT-004-2023 | 2nd March, 2023 at 10.00 am EAT |
| 3. | Supply of Jet A-1 Fuel for KETRACO Helicopter | KETRACO-PT-005-2023 | 1st March, 2023 at 11.00 am EAT |

KETRACO tenders run on SAP ARIBA e – procurement platform and therefore tender documents detailing the requirements may be viewed at KETRACO e-procurement portal found on the KETRACO website (***www.ketraco.co.ke***) starting from **Tuesday 14th February 2023.**

Tender enquiries, clarifications and/or addendums to ***pkubasu@ketraco.co.ke*** and ***lswaleh@ketraco.co.ke.*** Complete bid documents should be electronically submitted through SAP ARIBA platform on or before the closing dates.

Bids will be opened electronically promptly thereafter in the presence of the tenderers or their representatives who choose to attend in KETRACO Supply Chain Management Offices at KAWI House, South C, Nairobi.

**SENIOR MANAGER, SUPPLY CHAIN MANAGEMENT**
**FOR: Ag. MANAGING DIRECTOR**

KENYA VISION 2030



REPUBLIC OF KENYA
EPRA
Energy & Petroleum Regulatory Authority

## MWALIKO KUSHIRIKI TENDA

Energy and Petroleum Regulatory Authority (EPRA) ni shirika la kiserikali lilloanzishwa chini ya Sheria ya Kawi, 2019. Shirika hilo ndilo kisheria husimamia sekta ya kawi hasa kuhusiana na maswala ya kitaaluma na kiuchumi katika sekta ndogo za umeme, kawi safi, petroli na makaa.

Mamlaka inaalika maombi kutoka kwa taasisi zilizohitimu kushiriki tenda zifuatazo: -

| No. | Nambari ya Tenda | Maelezo ya Tenda | Washiriki | Siku ya mwisho |
|---|---|---|---|---|
| 1 | EPRA/SCM/4/3/22-23/083 | Ushauri kuhusu athari ya ripoti kielelezo kuhusu Kanuni za kuripoti Visa na Ajali, 2022 | WAZI | 7/3/2023 |
| 2 | EPRA/SCM/4/3/22-23/084 | Ushauri kuhusu Athari ya Tathmini kuhusu Utendakazi wa Vifaa vya Kawi na Kanuni za kuweka Lebo | WAZI | 7/3/2023 |
| 3 | EPRA/SCM/4/3/22-23/090 | Utoaji wa Huduma za Ulinzi | WAZI | 7/03/2023 |
| 4 | EPRA/SCM/4/3/22-23/092 | Kutathmini Utoshelevu wa Wateja na Hisia kuhusu Shirika | WAZI | 8/3/2023 |
| 5 | EPRA/SCM/4/2/22-23/087 | Kununua na kuleta Vipakatalishi | Imetengewa (vijana) | 1/3/2023 |
| 6 | EPRA/SCM/4/2/22-23/088 | Kununua, Kuleta, na Kutunza Sava | WAZI | 8/3/2023 |
| 7 | EPRA/SCM/4/3/22-23/085 | Kandarasi ya Utoaji wa Huduma za Tikiti za Ndege | Imetengewa (Wanawake) | 1/3/2023 |
| 8 | EPRA/SCM/4/3/22-23/086 | Kandarasi ya Utoaji wa Huduma za Mikutano na Malazi | WAZI | 9/3/2023 |
| 9 | EPRA/SCM/4/3/22-23/093 | Kunua, Kuunda na Kuweka mfumo wa kufuatilia Magari | WAZI | 9/3/2023 |

Stakabadhi za tenda zinaweza kupakuliwa kutoka kwa Wavuti wa EPRA **www.epra.go.ke** au kwenye lango la Public Procurement Information Portal (PPIP) **https://tenders.go.ke/website/tenders/Index**

**Mkurugenzi Mkuu**
**Energy and Petroleum Regulatory Authority**

KENYA VISION 2030

FEBRUARI 21, 2023

# MyGov.

NAIROBI-KENYA I TOLEO No. 32/2022-2023

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: info@information.go.ke

## Wakulima wapewa samaki 250,000 wa kufuga gavana akiwaahidi soko jipya

**NA IRUNGU MWANGI (KNA)**

Serikali ya kaunti ya Kirinyaga imesambaza samaki 254,000 wa kufuga lwa wakulima ili kupiga jeki uzalishaji kufuatia kuongezeka kwa matumizi ya samaki katika ukanda wa Mlima Kenya.

Samaki hao wa kufuga ambao walikabidhiwa wakulima 254, kila mmoja akipokea1,000, ni sehemu ya mpango mkubwa wa kaunti hiyo wa kuwawezesha wakulima kushiriki ufugaji wa samaki kama shughuli rasmi kinyume na kuuchukulia kama chanzo mbadala ya kujikimu kimaisha.

Ili kuunda soko kwa mavuno makubwa yanayotarajiwa ya samaki siku zijazo, serikali ya kaunti itajenga soko la samaki pekee katika Kiaga, eneo bunge la Ndia, ambako wakulima watakuwa wakipeleza zao lao kuuzwa.

Kwa miaka mitatu iliyopita, ufugaji wa samaki katika kaunti hiyo umekuwa ukiongezeka pole pole chini ya mpango wa uwezeshaji wa kiuchumi wa kaunti hiyo wa Wezesha Kirinyaga ulioanzishwa na Gavana Anne Waiguru.




Wafanyakazi wa kaunti ya Kirinyaga wasambaza samaki wadogo kwa wakulima wanaofuga samaki katika kaunti.



Mkulima aingiza samaki wadogo kwenye kidimbwi chake.
PICHA: IRUNGU MWANGI (KNA)

"Ukulima wa samaki utapatia wakulima wetu mapato za ziada na kusaidia wanawake na vijana ambao watahusishwa katika awamu tofauti za mradi huo wa uongezaji thamani," alisema Gavana Waiguru.

Alisema kwamba ufugaji wa samaki utapunguza uhaba mkubwa wa samaki ndani na nje ya Kirinyaga kwa kuwa nusu ya samaki wanaozalishwa Kenya wanatoka kutoka ufugaji na nusu wanavuliwa baharini na kwenye ziwa.

Waiguru alisema kwamba mojawapo wa viwanda vya kutengeneza samaki kitajengwa eneo la viwanda litakaloanzishwa Sagana na hivyo, kuna haja ya kuwa na mali ghafi nyingi kutoka eneo hilo. Wakulima wa samaki watanufaika zaidi kutoka kwa uongezaji thamani wa samaki wao.

Alisema kwamba maono yake ni kuona Kirinyaga ikinufaika na uwezo wa uvuvi ikizingatiwa kwamba ina hali nzuri ya ufugaji wa samaki kwa kuwa na maji yasiyochafuliwa na soko lilolo tayari.

Mkuu huyo wa kaunti alisema kwamba anataka kuongeza uzalishaji wa samaki kutoka tani 29.4 zenye thamani ya Sh12.8 milioni hadi tani 62 ambazo zitawapa wakulima takriban Sh30 milioni kwa mwaka.

Chini ya mpango wa uvuvi, serikali ya kaunti imekuwa ikisaidia wakulima kwa kuwapa vifaa vya uvuvi, samaki wa kufuga na chakula cha kuwalisha kwa miezi sita.

Kwa upande wao wakulima wanajenga vidimbwi vya kufugia samaki na kuwatunza samaki hadi wakomae.

## Jamii za Pwani zapigwa jeki ruzuku ya Sh109 milioni ikianzishwa Kwale

**NA HUSSEIN ABDULLAHI (KNA)**

Idara ya Serikali ya Uchumi wa Baharini na Uvuvi, kupitia Mradi wa Uvuvi Baharini na Maendeleo ya Uchumi Jamii Kenya (KEMFSED) imetoa ruzuku ya Sh109 milioni kwa miradi ya jamii kaunti ya Kwale.

KEMFSED ni mradi unaofadhiliwa na Serikali ya Kenya na Benki ya Dunia. Unasaidia nchi katika juhudi zake za kutumia nafasi ibuka katika sekta ya uchumi wa baharini.



Makundi ya Kutunza Mazingira Baharini eneo la Kwale yapokea ruzuku ya Sh 109 milioni kutoka kwa Idara ya Uchumi wa Baharini chini ya mradi wa KEMFSED.

Mradi huo wa mabilioni ya pesa unalenga kusaidia mipango katika viwango vya kijamii ya kutunza na kuirejesha mazingira ya baharini.

Sekta ya Uchaguzi wa Baharini inahusisha shughuli nyingi za uchumi miongoni mwa jamii za Pwani kama vile uvuvi, ufugaji wa samaki, uchukuzi wa baharini na utalii.

Mradi huo utatekelezwa hadi 2025 kwa wakati mmoja katika kaunti za pwani za Mombasa, Kwale, Kilifi, Lamu na Tana River kwa ufadhili wa Sh10 bilioni kutia nguvu ustahilimivu wa pwani.

Ruzuku inatolewa kutia nguvu shughuli za kujikimu kimaisha za jamii za Pwani kwa kuwezesha ubunifu, uongezaji thamani, kukuza biashara na kuongeza ajira. Vikundi 43 vya utunzi wa bahari vitanufaika katika awamu ya kwanza ya ufadhili wa uchumi wa baharini ulionzishwa katika hafla iliyoongozwa na Gavana Fatuma Achani katika makao makuu ya kaunti mjini Kwale.

## KWA UFUPI

### Duale ateuliwa kinara mpya wa kikosi Afrika Mashariki

Waziri wa Ulinzi, Aden Duale, ameteuliwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Kikosi cha Afrika Mashariki (EASF) katika mkutano uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia.

Duale alichukua uenyekiti wa Baraza hili kutoka kwa Waziri wa Ulinzi wa Ethiopia Dkt Abraham Belay ambaye muhula wake ulikamilika huku Brigedia Paul Njema wa Jeshi la Ulinzi la Kenya akiteuliwa Mkurugenzi wa Afisi ya EASF.

Mkutano huo pia ulikubaliana kwa pamoja kwamba Kenya iwe mwenyekiti wa Marais wa Nchi na Wakuu wa Serikali na Kamati ya Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi. Mkutano huo wa mawaziri ulitanguliwa na ule wa Kamati ya Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi wa nchi wanachama chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi wa Ethiopia Field Marshall Birhanu Jula Gelalcha.

Wakuu hao wa majeshi walisema kwamba hali ya usalama wa ukanda imebadilika muda unavyoendelea kusonga na kwamba kuna haja ya kuinua uwezo wa EASF zaidi ya kuwa kikosi cha kuwa tayari kwa lolote. Baraza hilo lilipendekeza kwamba EASF ijitathmini yenyewe kuona jinsi inaweza kuundwa kutimiza mahitaji ya changamoto za sasa za usalama. Kufanya hivi, washiriki walipendekeza kuanzishwa kwa Jopo la Wazee (PoE) ikisubiri uhalalishaji wake.

Afisi ya EASF ilisema kwamba Muungano wa Afrika (AU) umeonyesha nia ya kuanzisha Kituo cha Mafunzo ya Matibabu katika moja ya nchi wanachama wa EASF ambazo ni Burundi, Comoros, Djibouti, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Ushelisheli, Somalia, Sudan, na Uganda.

EASF ilianzishwa kama mpango wa kikanda wa kutoa uwezo wa majeshi kutumwa upesi kwa shughuli za kuzuia, kuleta uthabiti na kudumisha amani. Kikosi hicho ni cha kikanda kilicho na jukumu la kudumisha usalama na amani katika eneo la Afrika Mashariki na ni mojawapo wa vikosi vitano vinavyowekwa tayari vya Jeshi Afrika vinavyohusisha Jeshi, Polisi na raia.

Vikosi vingine kama hivyo barani Afrika ni cha Kaskazini (NARC), Kikosi cha Magharibi mwa Afrika (ECOWAS), Kikosi cha Kati ya Afrika (ECCAS) na Kikosi cha nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

*Na Bogita Ongeri (PCO)*

### Shirika la Bima lapanga kuinua ulinzi wa wateja

Mamlaka ya Kuthibiti Bima (IRA) imeanza mabadiliko yanayonuiwa kuhakikisha uthibiti bora wa sekta ya bima ili kukidhi mahitaji ya wateja na kutatua changamoto zinazoibuka. Mwenyekiti mpya aliyeteuliwa kusimamia mamlaka hiyo, Mwambu Mabonga alisema mabadiliko yanayoendelea yanalenga kufanya IRA kuendesha sekta inayokua haraka ya bima Kenya, kutekeleza jukumu lake kwa mujibu wa sera zilizopo za serikali.

Bw Mabonga, aliyechukua uenyekiti kutoka kwa Mohammed Sheikh Amin, alishukuru mtangulizi wake na Bodi ya IRA kwa kuongoza mchakato wa maendeleo, ambao aliahidi kuendelea kutekeleza hadi ufaulu.

"Ninajiunga na Mamlaka hii wakati ambao viongozi wenye maono wameanzisha kitakachobadilisha pakubwa bima nchini. Ninataka kuhakikishia bodi yote na using kwamba nitajitahidi kuafikia malengo yaliyowekwa kwa manufaa ya sekta ya bima," alisema Mabonga, alipotwaa rasmi uenyekiti kutoka kwa Bw Amin.

Alisema kwamba Mamlt inatayarisha mpango wake wa tano wa mkakati kutumika kutoka 2023 hadi 2027, kwa lengo la kuangazia zaidi ulinzi wa wateja na kuimarisha upatikanaji wa huduma za bima.

" Ukuaji bora na usiotatizika na upatikanaji wa bima hauwezi kuafikiwa wakati masuala ya upatikanaji, gharama na imani ya wateja zinabaki kuwa changamoto, na hii ndiyo Mpango huu wa Mkakati unalenga kushughulikia," alisema Mpango huo wa Mkakati, alisema, utapendekeza mikakati ya kutatua changamoto zilizoko huku IRA ikijitahidi kuweka hatua zinazolengwa kuinua bima na kulinda wanaoweka bima. Bw Mabonga alisema kwamba anafahamu kabisa changamoto zinazokumba sekta ya bima nchini, na akaahidi kushauriana kwa upana na wadau kwa lengo la kupata suluhu la kudumu la ukuaji wa sekta hiyo.

Alipongeza usimamizi kwa kuongoza Mamlaka hiyo hadi ilipo kwa wakati huu, akisema ufanisi wake haungeafikiwa bila timu ya watumishi wa umma iliyojitolea.

*Na Maripota wa MyGov*

REPUBLIC OF KENYA
GAA GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY
KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD

**DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD**
NHIF Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100
Tel: 0202715390 / 0757029456
Email: info@kenyayearbook.go.ke
www.kenyayearbook.co.ke